
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA MAALUM

TOLEO LA APRILI 2021

## NSSF yatoa elimu kwa sekta isiyo rasmi katika Maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi, jijini Mwanza.



Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

www.nssf.or.tz

Simu Bure 0800116773

customercare@nssf.or.tz

@NssfTanzania

# NSSF YAWAFIKIA WAJASIRIAMALI KATIKA MAONESHO YA OSH - MWANZA

300 wapatiwa Elimu, 45 wasajiliwa




**Na MWANDISHI WETU**

Wajasiriamali 300 walipatiwa elimu ya Hifadhi ya Jamii katika Maonesho ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi ambapo wajasiriamali 45 walijiunga na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) yaliyofanyika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Akizungumzia ushiriki wa NSSF kwenye maonesho hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Masha Mshomba, alisema walifanikiwa kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa wajasiriamali mbalimbali waliopo kwenye sekta isiyo rasmi pamoja na kuwaandikisha.

Mshomba alisema kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, Mfuko umepewa jukumu la kuandikisha wanachama kutoka sekta rasmi na sekta isiyo rasmi kama wakulima, wavuvi, wafugaji, wachimbaji wadogo, bodaboda na mamalishe; kwamba baada ya kujiunga watanufaika na mafao yote yanayotolewa na Mfuko huo.

“Kazi ya kuwasajili wananchi walio katika sekta isiyo rasmi tunaifanya kwa jitihada kubwa na tumejiwekea mikakati ya kuwasajili watu wote ambao wanastahili kusajiliwa ikiwemo kuwapatia elimu,” alisema Mshomba.

Alisema Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, katika hotuba yake aliyoitoa Aprili 6, mwaka huu, aliiagiza NSSF kuhakikisha inaandikisha watu waliopo katika sekta isiyo rasmi na kwamba agizo hilo limewekewa mikakati kwa ajili ya utekelezaji.



Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kushoto) akimhudumia mwanachama wa sekta isiyo rasmi (kulia) alipotembelea banda la Mfuko huo katika Maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

# NSSF KULETA NEEMA SEKTA ISIYO RASMI

**Na MWANDISHI WETU**

Yajayo yanafurahisha! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwenda kuandika historia nyingine ambapo safari hii ni kwenye sekta isiyo rasmi kwani Mfuko unatarajia kuzindua mpango kabambe ambao utaleta neema na faraja kwa sekta hiyo.

Kauli hiyo ya kutia moyo ilitolewa hivi karibuni, wakati wa Maonesho ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, ambaye alisema kuwa ndani ya mwezi mmoja wanatarajia kuzindua mpango huo ambao utakuwa mkombozi mkubwa kwa wajasiriamali watakaojiunga na Mfuko huo.

Akifafanua zaidi kuhusu mpango huo, Meneja wa NSSF Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Kahensa, alisema hivi karibuni wanatarajia kuzindua kampeni kubwa ya kuelimisha watu waliopo katika sekta isiyo rasmi, na kwamba tayari wanaendelea na mazungumzo na chama cha waendesha bodaboda nchini.

Kwa mujibu wa Kahensa, katika sekta isiyo rasmi moja ya mafao ambayo watatoa ni kumuwezesha mwanachama kujipatia kipato, akitolea mfano mtu ambaye anajishughulisha na bodaboda basi atapatiwa pikipiki ambayo atailipa kwa utaratibu utakaowekwa.

Alisema mikopo hiyo itatolewa na NSSF kupitia benki ya Azania, ambapo aliwahamasisha wajasiriamali wote kujiunga na Mfuko huo ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali ambazo zitatolewa hivi karibuni.

Katika hatua nyingine, Kahensa alisema NSSF inatarajia kutoa fao la matibabu kwa wanachama wake katika muda mfupi ujao baada ya taratibu kukamilika, lengo ni kuwapunguzia gharama za matibabu Watanzania.



*Maafisa wa NSSF wakitoa elimu kwa wajasiriamali.*

# 4 KALI ZILIZOBAMBA



**Masha Mshomba**
Mkurugenzi Mkuu wa NSSF

*Mfuko uko vizuri sana katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kulipa mafao na kwa mujibu wa hesabu zetu za mwezi Disemba mwaka 2020, thamani ya Mfuko ni Shilingi Trilioni 4.8, hivyo tunaweza kutekeleza majukumu yetu kwa kipindi cha miaka 70 inayokuja.*



**Emmanuel Kahensa**
Meneja wa NSSF Mkoa wa Mwanza

*Kupitia maonesho yale, Mfuko ulitoa elimu kwa wajasiriamali takribani 300, kati yao 45 waliandikishwa na kuwa wanachama wa NSSF.*



**Inaaya Riwa**
Afisa Matekelezo Sekta isiyo rasmi Mwanza.

*Fao hili la uzazi linatolewa kwa mwanachama mwanamke pale atakapojifungua, ambapo anatakiwa kuwa amechangia kwa kipindi kisichopungua miezi 36 na kati yake iwe michango ya miezi 12 iliyowasilishwa karibu na wiki ya kujifungua.*



**Seif Pepo**
Afisa Matekelezo NSSF Mwanza

*Natoa wito kwa waajiri kulipa michango ya wanachama mapema kama Sheria inavyotaka, mwajiri kulipa michango mapema anaurahisishia Mfuko kuondoa changamoto za mwanachama za kuchelewa kulipwa.*

# NSSF YAWAONYA WAAJIRI WASIOLIPA MICHANGO KWA WAKATI



**Na MWANDISHI WETU**

Waajiri nchini wametakiwa kutimiza takwa la kisheria la kulipa michango ya wafanyakazi wao ili watakapostaafu au kupata janga lolote, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), uweze kuwalipa kwa wakati.

Afisa Matekezo wa NSSF Mkoa wa Mwanza, Seif Pepo, alitoa wito huo wakati wa Maonesho ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi, yaliyofanyika hivi karibuni jijini Mwanza.

Alisema mwajiri kulipa michango ya wafanyakazi wake kwa wakati anaurahisishia Mfuko kuondoa changamoto za mwanachama za kuchelewa kulipwa kwamba anapostaafu au kupata janga kama michango yake yote ipo vizuri mwanachama huyo atalipwa haraka bila ya usumbufu.

Pepo alisema jukumu la mwajiri ni kulipa michango mapema na kwamba mwanachama anawajibu wa kutoa taarifa NSSF iwapo kuna changamoto yoyote ya kutopelekewa michango ili Mfuko uweze kumchukulia hatua mapema mwajiri husika.

Kuhusu maonesho hayo, Pepo alisema walikuwa wanatoa elimu kwa waajiri kuhusu ulipaji wa michango, walikuwa wakitatua changamoto mbalimbali za wanachama na waajiri, kuandikisha wanachama na kutoa elimu kwa wajasiriamali kuhusu sekta isiyo rasmi.



# HABARI KATIKA PICHA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Jenista Mhagama, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alipotembela banda la NSSF katika maonesho ya wiki ya usalama na afya mahali pa kazi, viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza.*



*Baadhi ya wafanyakazi wa NSSF wakishiriki maandamano katika kilele cha siku ya wafanyakazi duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mwanza katika viwanja vya Nyamagana.*



*Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kulia) akitoa maelezo mafupi mbele ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Mhe. Patrobas Katambi (kushoto) alipotembelea banda la Mfuko huo katika Maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi.*

*Afisa Matekezo wa NSSF Mkoa wa Mwanza, Seif Pepo,(kushoto) akimhudumia mwanachama wa NSSF (kulia) aliyetembelea banda la Mfuko huo katika Maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi yaliyofanyika hivi karibuni, viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza.*



# NSSF YATANGAZA FURSA KWA WAJASIRIAMALI



*Afisa Matekelezo wa NSSF, Mkoa wa Mwanza, Inaaya Riwa (kulia) akimuandikisha mjasiriamali (kushoto) aliyetembelea banda la NSSF na kuamua kujinga mara baada ya kupatiwa elimu ya Hifadhi ya Jamii.*

**Na MWANDISHI WETU**

Afisa Matekelezo wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Mwanza, Inaaya Riwa, amewahamasisha wajasiriamali kujiunga na Mfuko huo ili waweze kunufaika na mafao mbalimbali.

Kwa mujibu wa Inaaya, kwa wajasiriamali waliopo katika sekta isiyo rasmi, NSSF inatoa mafao mbalimbali kwa watakaojiunga yakiwemo ya uzeeni kwa yule ambaye atachangia miezi 180 au miaka 15, mafao ya matibabu ambayo yanatolewa kwa mwanachama atakayechangia ndani ya miezi sita mfululizo na fao la uzazi.

“Nawashauri wajasiriamali wote mama lishe, bodaboda, wavuvi, wakulima kujiunga na NSSF kwani inawajali imeleta mafao bora kwao, hivyo wanapaswa kujiunga ili kujiwekea akiba yao kwa maisha ya sasa na ya baadaye,” alisema.

Inaaya alisema fursa nyingine ambazo watu waliopo katika sekta isiyo rasmi ambao watajiunga na NSSF watanufaika nazo ni pamoja na mikopo midogo midogo, inayotolewa kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo na vya kati.

Mikopo hiyo inatolewa kupitia mpango maalumu wa SANVN Viwanda Scheme, walengwa wakiwa ni wajasiriamali wadogo na wa kati waliopo katika sekta ya viwanda wenye lengo la kuanzisha au kuongeza uzalishaji na kwamba inatolewa kwa ushirikiano baina ya VETA, SIDO, NEEC, Benki ya Azania na NSSF.

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF